***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA NJOMBE

**MTIHANI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA SITA**

**121/1** **KISWAHILI 1**

**(Kwa Watahiniwa wa Shule na Kujitegemea)**

**MUDA: SAA 03: 00** **JUMATANO, 13 Machi 2024 Mchana**

**MAELEKEZO KWA MTAHINIWA**

1. Mtihani huu una sehemu **A**, na **B** zenye jumla ya maswali (08)
2. Jibu maswali (07)
3. Jibu maswali yote sehemu **(A)** na maswali **matatu (03)** sehemu **(B)**
4. Swali la saba ni la lazima.
5. Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.
7. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.

## SEHEMU A (Alama 40)

**1.** Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa makini kisha jibu kwa usahihi maswali yanayofuata.

Kipindi cha kuanzia mwaka **1930** hadi **1938** kilikuwa muhimu sana kwa historia ya usanifishaji wa Kiswahili.

Mambo mbalimbali yalifanyika ili kuhakikisha kuwa kinasitawi na kushamiri. Kuundwa kwa kamati maalumu ya kushughulikia lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, ilikuuwa hatua muhimu sana katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili.

Kazi za kamati ya lugha ya Afrika Mashariki zilikuwa nyingi kama vile, kusanifisha otografia itakayotumika kwa watumiaji wote wa Kiswahili, kuandaa kamusi mbalimbali, kutoa hamasa kwa waandishi wachanga wanaotumia lugha ya Kiswahili katika kuandika kazi zao, kusahihisha lugha katika vitabu vilivyokuwa vinatumika kufundishia shuleni na kufanya tafiti mbalimbali za lugha ya kiswahili.

Kamati ya lugha ya Afrika Mashariki ilifanya kazi chini ya usimamizi wa utawala wa mwingereza. Kazi za kamati Zilipamba moto huku tafiti mbalimbali kuhusu lahaja za Kiswahili zikiendelea kufanyika. Tafiti hizo zilizaa matunda na hatimaye ikaonekana ni vizuri kuchagua lahaja moja na kuisanifisha ili iwe msingi wa kiswhili sanifu.

"Mungu hamtupi mja wake" Sudi iliangukia kwa lahaja ya kiunguja na ilichaguliwa kuwa lahaja ya Kiswahili sanifu.Watumiaji wa lahaja zingine walikuwa na inda baada ya lahaja ya kiunguja kutangazwa kuwa msingi wa usanifishaji wa Kiswahili. Kamati haikufanya ajizi, ilianza mara moja kazi ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Kiswahili sanifu tukitumiacho leo ni matunda ya kazi ya utawala wa waingereza katika usanifishaji wa lahaja ya kiunguja.

Kwa ujumla tunaweza kusema kati ya Wakoloni wote, Wakoloni wa Kiingereza ndio waliofanya kazi kubwa katika kukuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Kupitia sera na mfumo wa utawala wa wakati huo walifanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na kuenea katika nchi za Africa Mashariki.

Maswali:

(a) Toa maana ya maneno yafuatayo;

i. Usafishaji
ii. Kamati
iii. Sudi
iv. Inda
v. Hamasa
vi. Sera.

(b) Andika kichwa cha habari uliyoisoma kisichozidi maneno matatu.

(c) Mwandishi ana maana gani anaposema "Mungu hamtupi mja wake"?

(d) Fupisha habari ifuatayo kwa kutumia maneno mia moja.

Wewe ni mwenye hasira nakupa shauri langu kuwa hutaweza kuishi katika dunia hii kama huondoi huzuni yako ukacheka. Kicheko ni furaha, mwache masikitiko apite mbali nawe. Cheka upate tokwa na uchungu, kwani hicho huondoa mikunjo ya uso wala si mchina au alovera. Cheka uondoe uchovu, cheka waone sura.Inuka usimame wima, usigaegae chini.

Simama wima tena cheka ili mchezo upate Kuendelea kwa shangwe na yowe la kicheko chako kikubwa. Kicheko ndicho kitu kitoshacho kwa mtu.Futa huzuni katika uso wako ucheke. Uishi miaka nenda. Mungu alieumba ulimwengu mchezo wake ni furaha. Alipoumba mbingu ya sita na kisha ya saba akacheka kicheko. Dawa ya huzuni ni kicheko, ukicheka itakimbia.

Na iwe kawaida yako kucheka mchana, asubuhi, joini, ili damu yako itembee. Ndiyo kicheko dawa ya msiba na mkeo au mmeo akikupa kisogo, cheka udumu kijana, cheka uuze sura, cheka uite vijana, cheka ukaribishe vijana, cheka wajukuu wacheke. Cheka ushinde vyote. Dawa ya nguvu mwilini, kicheko; Ni sumu katika maisha na inafaa kujitenga na huzuni, kicheko kiwe blanketi na shuka la kukumbatia, cheka kicheko kwa nguvu pamoja na malaika wema walio katika mbingu, makusudi moyo wako uweze kuwa mweupe. Ondoa shaka moyoni ucheke na zamu yako ya heri itakuja. Ah! msinichoshe mtoto wa mwenzenu, nikachekee nje….!

2. (a)Eleza maana ya kishazi huru.
   (b) Katika lugha ya Kiswahili kishazi huru hujipambanua kikiwa katika miundo mbalimbali; Onesha miundo mitano ya kishazi huru kwa mifano maridhawa.

3. Wataalamu mbalimbali wa Isimu ya lugha husema "hakuna utata katika lugha, isipokuwa uwezo wa kuondoa utata huo upo kwa watumiaji husika" Thibitisha usemi huu kwa hoja tano.

4. Kwa kutumia mifano dhahiri, Onesha maumbo matano ya utokeaji wa mofu ya kauli ya utendesheshi.

**SEHEMU B (Alama 60)**

**Jibu maswali matatu (03) kutoka sehemu hii, swali la saba (07) ni la lazima.**

5. Jifanye wewe ni mjasiriamali unauza mitumba sokoni mkuyuni. Andika barua ya kuomba mkopo kutoka Benki ya MKOMBOZI. Jina lako liwe shida zitaisha S.L.P 1120 liwale,Lindi.

6. Kuteuliwa kwa lahaja moja ya usanifishaji wa lugha hupelekea lahaja nyingine kudumaa. Jadili sababu ambazo zimepelekea kudumaa kwa lahaja nyingine mara baada ya kuteuliwa kwa lahaja ya kiunguja. (toa sababu tano (05).

7. Ujio wa wakoloni nchini Tanzania ulisaidia kwa kiasi kikubwa katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili kupitia shughuli zao mbalimbali, lakini kwa upande mwingine walikidumaza kiswahili. Thibitisha jinsi waingereza walivyodumaza lugha ya kiswahili nchini Tanzania.

8. Taaluma ya tafsiri ina umuhimu mkubwa sana katika maisha ya kila siku ya binadamu fafanua kwa mifano kauli hii kwa kutumia hoja tano.